**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 3 No. 2 (2025): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v3i2.1452


# Maisha ya Penina Muhando na Mchango wake katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili

**Anna N. Kyamba**
*Chuo Kikuu Huria cha Tanzania*

***Uwasilishaji wa Makala***
Kupokelewa: 2025-05-19
Kurekebishwa: 2025-11-17
Kukubaliwa: 2025-11-20
Kuchapishwa: 2025-11-23

**Maneno Muhimu**
Fasihi
Kiswahili
Sanaa
Tamthiliya

***Jinsi ya Kurejelea Makala:***
Kyamba, A. N. (2025). Maisha ya Penina Muhando na Mchango wake katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili. *Journal of Kiswahili and Other African Languages, 3*(2), 99-107.

Copyright © 2025
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Penina Muhando ni mwanazuoni aliyetoa mchango mkubwa katika maendeleo ya fasihi na lugha ya Kiswahili. Mchango wake umeonekana hasa katika tamthiliya, sanaa za maonyesho pamoja na thieta ya umma ama sanaa kwa maendeleo ya jamii. Vitabu vyake vya tamthiliya vimeonesha namna alivyochangia katika maendeleo ya tamthiliya kwa kuanzisha mbinu ya usimulizi wa kingano katika tamthiliya zake pamoja na thieta ya umma ili kusadifu utamaduni wa Kibantu. Pia, amesaidia katika kukuza lugha ya Kiswahili kwa kuongeza msamiati kupitia utunzi wake. Licha ya mchango wake huo katika tamthiliya na sanaa za maonyesho, mwandishi huyu hajachunguzwa kinagaubaga ili kubaini mchango wake katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Watafiti mbalimbali wamechunguza baadhi ya kazi zake na kumtaja kuwa ana mchango mkubwa katika fasihi pasipo kuchambua mchango huo (Mutembei 2008; Msemwa 2012 na Sayi 2023). Kutokana na umuhimu wa mtaalamu huyu katika uwanja wa fasihi, hususani katika uwanja wa tamthiliya, ndipo makala hii inakusudia kuchunguza maisha ya Penina Muhando na mchango wa kazi zake katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Data zilizomo ndani ya makala hii zimetokana na usomaji makini wa kazi zake pamoja na mahojiano baina ya mtafiti na mtafitiwa nyanjani kuhusu mchango wake katika fasihi ya Kiswahili. Makala hii inaongozwa na Nadharia ya Uhalisia iliyoibuka karne ya 19 ili kupinga Tapo la Uromansia. Nadharia hii inasisitiza usawiri wa matukio au maisha katika fasihi kama yalivyo katika maisha ya kila siku. Kupitia nadharia hii tumebaini kuwa Penina Muhando amechangia kukuza fasihi ya Kiswahili kwa kutumia lugha ya Kiswahili, kuingiza maudhui ya dini za Kiafrika katika fasihi na kuhamasisha masuala ya usawa wa kijinsia. Kadhalika, mwanzilishi wa Thieta ya Umma, fasihi ya majaribio ya Kiafrika pamoja na nadharia za fasihi ya Kiswahili.

## Utangulizi
Makala hii imeshughulikia mchango wa Penina Muhando[1] katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Watafiti mbalimbali wamechunguza kazi za Penina Muhando kwa namna mbalimbali. Baadhi ya watafiti hao ni Mutembei (2008 na 2012), Nicholaus (2011), Msemwa (2012), na Sayi (2023). Watafiti hawa wanadokeza kuwa Penina Muhando ana mchango mkubwa katika fasihi ya Kiswahili.

[1]Pia nimetumia Muhando nikimaanisha Penina Muhando.

Mathalani Sayi (2023) anaeleza kuwa utafiti wake unatoa mchango katika maendeleo ya fasihi, hususani tamthiliya ya Kiswahili kwa kujadili taswira zilizotumika katika tamthiliya ya *Nguzo Mama* na ujumbe unaoibuliwa na taswira hizo. Tafiti nyingi zilizofanywa zikihusisha tamthiliya ya *Nguzo Mama* zimeshughulikia masuala ya usawiri wa mwanamke (Mule, 2004; Caleb, 2015; Mapunjo, 2014; George, 2014). Aidha, watafiti wengi waliotangulia wamejikita katika kuchunguza tamthiliya za Penina Muhando katika vipengele vya fani, maudhui, korasi, na falsafa. Kwa mfano, Msemwa (2016) alikusudia kuangazia mchango wa Penina Muhando katika tamthiliya, lakini isivyo bahati alivyoanza tu utafiti wake, alifariki. Mutembei[2] (2016) (katika maombolezo ya Kelvin Msemwa) alieleza kuwa "Msemwa alikusudia kufanya utafiti kuhusu mchango wa Penina Muhando na kushauri watafiti wafanye utafiti kumhusu mtaalamu huyu ili mchango wake ujulikane". Hadi sasa hakuna utafiti ulioshughulikia kikamilifu historia ya maisha yake na mchango wa mwandishi huyu katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Baadhi ya watafiti wameishia kudokeza tu mchango wake katika kazi zao pasi na kufanya uchambuzi. Watafiti hao ni Mutembei (2008), Msemwa (2012), Mapunjo (2014), Mulokozi (2017) na Sayi (2023). Kutokana hizo tumepata msukumo wa kuandika makala hii ili kubaini mchango wa mtaalamu huyu katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili kwa kuongozwa na Nadharia ya Uhalisia.

## Nadharia ya Uhalisia

Nadharia hii iliibuka karne ya 19 na kufafanuliwa zaidi na Erving Goffman aliyeishi kati ya mwaka (1922 - 1982). Baadhi ya wataalamu wanaotoa mchango wao kuhusu Nadharia ya Uhalisia ni Gustav Flaubert (1846), Macdowall Arthur (1918), Rene Wellek (1960), George Lukacs (1963), na Georg Hegel (1979). Wanauhalisia hawa wanaamini kwamba fasihi inapaswa kuyasawiri maisha kama yalivyo, bila kupotosha wala kutia chumvi, huku ikijikita katika kuonyesha mahusiano na migongano ya kijamii, na matatizo na matamanio ya mtu wa kawaida katika hali ya kawaida ndani ya jamii. Lukacs (1963) anaeleza kuwa mwandishi anasukumwa kuusawiri uhalisia katika ukamilifu na kwa wakati wake maalumu. Nadharia ya uhalisia hujihusisha na kuchunguza undani wa picha inayoonekana ya uhalisi na kugundua sheria za mabadiliko ya kihistoria zinazoisababisha hali hiyo. Kutokana na maoni ya mtaalamu huyu inaonesha kuwa mwanafasihi ama mwandishi ana jukumu kubwa la kuuelewa ulimwengu kama kitu changamano na kinachobadilika. Anafafanua zaidi kuwa tukio, mhusika au mandhari huelezwa kihalisia ikiwa vinafanana na sura fulani ya maisha. Naye Wamitila (2002) anaeleza kuwa uhalisia unasisitiza usawiri wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Hili tunaliona kupitia kazi za Penina Muhando ambazo zinatoa picha za wahusika, matukio, na mandhari ambayo yanaoana kwa kiasi kikubwa na uhalisia wa jamii ya mwandishi anayehusika. Fasihi yoyote lazima ionekane kama kioo cha jamii (Wamitila, 2003). Hivyo basi, lazima jamii iweze kujitazama na kujiona kupitia fasihi ambayo ni zao la jamii. Msingi wa nadharia hii ni kuwa: Mosi sanaa iwakilishe ukweli na kuwakilishwa kwa maneno halisi. Pili, sanaa iwe aminifu na ionyeshe hali halisi ya mazingira. Nadharia hii imetumika ili kubainisha mchango wa Penina Muhando katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili, ambapo kupitia nadharia hii, tumeona namna mwandishi alivyoangazia mambo mbalimbali kwa kuakisi hali halisi ya jamii yake. Awali ya yote tuangazie kwanza methodolojia iliyotumika katika makala haya.

## Methodolojia

Data za makala hii zimepatikana kwa njia ya usomaji makini wa kazi mbalimbali za Penina Muhando kama vile *Hatia*, *Heshima Yangu*, *Tambueni Haki Zetu*, *Nguzo Mama,* na *Lina Ubani*, wasifu[3]

[2]Mutembei ni Profesa Mshiriki katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Taasisi za Taaluma ya Kiswahili (TATAKI). Pia alikuwa msimamizi wa Marehem Kelvin Msemwa kwenye utafiti wa Uzamivu.
[3]Wasifu hu ulipatikaa katika mahojiano yaliyofanyika mwaka 2020.

wake, pamoja na mahojiano yaliyofanyika baina ya mtafiti na mtaalamu huyu Januari 2020[4]. Kupitia njia hizo zimetuwezesha kupata historia ya maisha yake na mchango wake katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili, hususani katika uwanja wa Tamthiliya. Data zimewasilishwa kwa kutumia mkabala wa kitaamuli (maelezo). Kwa kuwa mtaalamu huyu amejikita zaidi katika uandishi wa tamthiliya na kazi nyingine za sanaa za maonyesho, kabla ya uchumbuzi wa mchango wake, kwanza tumeangazia kwa kifupi historia ya Penina Muhando.

**Historia ya Penina Muhando**

Penina Muhando[5] alizaliwa tarehe 03 Machi 1948 huko Berega, Wilaya ya Kilosa, Mkoani Morogoro. Penina Muhando anajulikana pia kama Penina Mlama. Baba yake aliitwa Oniviel Muhando na alikuwa mwalimu. Penina Muhando alisoma shule tofauti na vijiji tofauti kutokana na kuhamishwa baba yake kila baada ya mwaka mmoja. Kwa mfano, darasa la kwanza alisoma Berega, darasa la pili kijiji cha Mtega Milimani mkoa wa Morogoro. Darasa la Tatu alihamia Kisitu mkoa wa Morogoro, darasa la Nne alisoma kijiji cha Mamboya kijiji Morogoro. Baadaye, alihamia Dodoma, huko Mvumi (middle school) ambako alisoma darasa la tano hadi la nane. Kidato cha kwanza hadi cha nne alisoma Msalato huko Dodoma. Kidato cha tano na sita alisoma Jangwani Dar es Salaam. Baadaye alijiunga na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kusomea Shahada ya Kwanza katika Sayansi ya Jamii (Ualimu) alihitimu 1971 na Shahada ya Pili alihitimu 1973 na ya Tatu alisoma Sanaa ya Ukumbini kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kuhitimu 1983. Baada ya kumaliza masomo ya chuo mwaka 1971, aliajiriwa katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1971 kama Mkufunzi Msaidizi na aliendelea hadi kuwa Profesa upande wa Sanaa za Ukumbini. Aliwahi kuwa mkuu wa Idara za Sanaa za Ukumbini, Msaidizi wa Mkuu wa Kitivo cha Utafiti wa Sanaa za Ukumbini na baadaye alikuwa Mkuu wa Kitivo hicho. Vilevile, alikuwa Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma na kuwa mwanamke wa kwanza kushika nafasi hiyo katika Chuo hicho.

Mwaka 1996 hadi 2000 alianzisha TUSEME iliyonahusika kuwainua watoto wa kike katika shule za wasichana nchini Tanzania. Baadaye alifanya kazi katika shirika la 'Forum for African Women in Education' (FAWE), shirika hilo lilihusisha nchi 14 zilizokuwa kusini mwa Jangwa la Sahara. Baada ya miaka tisa alirudi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Mwaka 2011 aliteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Kigoda cha Mwalimu Julius Nyerere hadi alipostaafu 2018. Kwa sasa Penina Mhando ni mratibu wa utoaji Tuzo ya Kigoda hicho. Uandishi wake, Penina Muhando ameandika kazi mbalimbali za tamthiliya kama vile: *Hatia* (1972), *Tambueni Haki Zetu* (1973), *Heshima Yangu* (1974), *Pambo* (1975), *Talaka si Mke Wangu* (1976), *Nguzo Mama* (1982), na *Lina Ubani* (1984). Pia, aliandika kazi nyingine kwa kushirikiana na wandishi wengine zijulikanazo kama *Harakati za Ukombozi* (1982), *Tujue Kuhesabu (*1983), *Abjadi Yetu* (1983) *Ayubu* (1984), na *Fasihi na Sanaa za Maonyesho (*1977). Kazi nyingine ni *Gender Responsive Pedagogy: A Teacher's Handbook* (2005), *Empowering Youth through TUSEME, Let us Speak Out: A Teacher's Handbook* (2005), *The Gender Responsive School: A Handbook for Education Practitioners* (2005), *Culture and Development: The Popular Theatre Approach in Africa* (1991). Pia, ameandika makala mbalimbali za kitaaluma na zisizo za kitaaluma. Muhando amechangia sana katika kukuza taalma ya Kiswahil kama tuonavyo hapa.

[4]Mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti na Penina Muhando nyumbani kwake Kunduchi, Dar es Salaam, Januari 2020.

[5]Anajulikana pia kama Penina Mlama, jina la Mlama ni la mume wake na limetumika katika baadhi ya kazi zake. Penina Muhando limetumika zaidi katika kazi za kifasihi. Katika machapisho ya kitaaluma alikuwa tayari ameshaolewa, hivyo alitumia jina la Mlama.

**Mchango wa Penina Muhando katika Maendeleo ya Fasihi ya Kiswahili**
Penina mhando ni mwandishi wa kazi za fasihi hususani tamthiliya. Mwandishi huyu amechangia sana maendeleo ya fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania. Mchango wake unaonekana hasa katika vipengele vifuatavyo:

**Matumizi ya Lugha ya Kiswahili**
Matumizi ya lugha ya Kiswahili katika utunzi wa kazi za fasihi ni mojawapo ya kipengele muhimu sana katika kukuza na kuendeleza fasihi ya Kiswahili. Muhando amechangia kukuza fasihi ya kiswahili kwa kutumia lugha ya Kiswahili katika uandishi wa kazi zake, hususani tamthiliya za Kiswahili na kazi nyingine za kitaaluma. Baadhi ya vipengele vya lugha alivyotumia Penina Muhando katika kazi zake ni taswira za kugusa, kuonja, kuona, kufikirika, na nyinginezo. Mathalani, katika tamthiliya ya *Nguzo Mama* kuna taswira nyingi. Baadhi ya taswira hizo ni Patata, Nguzo Mama, Madigrii, na Chizi. Kwa mfano, taswira ya “Patata” (uk. 2-4) inatupatia picha ya mawazoni au kufikirika. Taswira hii inamfanya hadhira awaze juu ya kijiji ambacho kina ustawi mzuri na watu wema wa roho. “Nguzo Mama” inatupatia taswira ya kuhisi na kuona taashira ya umoja wa wanawake, kupitia taswira ya “Madigrii” (uk. 26-28), tunapata picha dhahania (kuhisi) ya elimu au usomi. Taswira ya mhusika “Chizi” tunapata picha ya kuhisi na kuona chizi anavyoonekana, mchafu mwenye mavazi na nywele chakavu, uchafu wa mazingira anayoishi na matendo yake. Vilevile, kupitia taswira hizo tunapata maudhui mbalimbali ya kisiasa, kijamii, na kiuchumi. Uteuzi wa taswira hizi unatokana na elimu yake pamoja na ujuzi wa lugha ya Kiswahili alionao. Mathalani, lugha iliyotumika katika *Lina Ubani* ni ya kawaida na yenye kueleweka. Ametumia tamathali za semi kama vile sitiari, tashibiha, na misemo (kur. 19, 35, 36, na 46). Pia, ametumia methali (uk. 36 na 46). Kadhalika, ametumia ukengeushi. Kwa mfano, “Lina ubani” inatokana na methali isemayo ‘La kuvunda halina ubani’. Hapa mwandishi alitumia ukengeushi kuonyesha kwa vile ambavyo tunaona havifai vinaweza kufaa mfano kupitia mhusika Mwanahego, Bibi na Huila. Wahusika hawa licha ya kwamba walionekana katika jamii hawana maana sana lakini ndio wamewezesha kufikisha jumbe husika. Muhando ametumia mbinu ya ukengeushi kuibua maudhui ya kijamii, kisiasa na kiuchumi. Pia, kuna matumizi ya lugha ya Kikagulu katika onyesho la kwanza, la tatu, na la sita. Vilevile, ametumia lugha ya Kiingereza katika Onyesho la pili na la nne. Kwa kufanya hivyo anaonesha mwingiliano wa kijamii unaoakisi uhalisia wa maisha. Kama asemavyo Wamitila (2002) kuwa uhalisia unasisitiza usawiri wa maisha ya jamii kwa uaminifu na usahihi mkubwa. Hali hii huchochea ubunifu kwa waandishi chipukizi ambao huandika kazi mbalimbali za fasihi ya Kiswahili kwa kusawiri hali halisi za kijamii.

**Kuchochea Ubunifu kwa Waandishi Chipukizi**
Uunifu ni dhana inayotumiwa kuelezea hali ya kuunda kazi zafasihi au kubuni na kandika kazi fulani (Wamitila 2003). Katika mahojiano yaliyofanyika mwaka 2020 Mhando alieleza chanzo cha kuwa mbunifu kulitokana na kupenda kwake kusoma pamoja na shule aliyosoma ilihimiza na iliweka utaratibu wa kusoma vitabu kwa kuwekewa nyota, kuanzia nyota nyeupe hadi ya kijani kwa aliyesoma vitabu vingi. Pia walihimizwa kutunga vitabu vya hadithi pamoja na kufanya drama akiwa shuleni. Pia alieleza kuwa kupitia hadithi alizosimuliwa na bibi yake kutokana na umahiri wake katika kusimulia hadithi mbalimbali za kusisimua, hadithi hizo zilimpatia msingi mkubwa wa kupenda drama. Kutokana na hilo, ndio maana ametumia mhusika Bibi akimsimulia Mota katika tamthiliya ya *Lina Ubani* kwamba Mota alitumia mbinu ya kishairi, hususani ushairi wa ngonjera kutunga hadithi alizomsimulia mama yake (uk. 55). Ubunif huo ulitokana na hadithi alizosimuliwa na Bibi yake. Hapa mwandishi anaakisi uhalisia wa maisha yake na mazingira halisi za jamii za kibantu. Mwandishi huyu kupitia kazi zake, amechochea bunifu kwa wanafunzi wake ambao wameandika tamthiliya za Kiswahili kama vile *Chungu cha Mwari wa Giningi* ya Shani

Kitogo (2005), *Safari ya Chinga* ya Shani Omari (2009) na *Changamoto* ya Elizabeth Mahenge (2010). Naye, Lukacs (1963) anaeleza kuwa mwandishi anasukumwa na njia ya kuusawiri uhalisia katika ukamilifu na wakati wake maalumu. Kwa ujumla, kupitia uhalisia wa maisha katika jamii tunapata maudhui mbalimbali kuhusu maisha.

**Kuingiza Maudhui ya Dini za Kiafrika katika Fasihi**

Penina Muhando ambaye ni Mkristo ametunga tamthiliya zake kwa kujiegemeza katika dini za kijadi. Kwa msingi huo, amechangia katika kuelimisha jamii kuenzi na kuthamini dini zetu za kijadi. Katika tamthiliya zake ameandika kuhusu kuwapo kwa dini hasa dini za kijadi ambazo zinazingatia kuwepo kwa mizimu na mzimu. Mizimu hufafanuliwa kuwa ni kivuli kinachosalia baada ya kifo cha mwanadamu (Mbiti, 2011). Katika Ontolojia ya Kibantu kuna imani ya kuwepo kwa ulimwengu wenye matabaka matatu, yaani duniani, kuzimu, na mbinguni. Mbiti anaeleza kuwa kwa Wabantu, huwa kuna uhusiano kati ya waliohai na wafu kwa sababu wahenga husaidia katika masuala ya familia, mila, maadili, na kazi. Watu wanapopata matatizo huomba msaada kutoka kwa miungu. Penina Muhando ameingiza maudhui ya dini za kijadi ambazo zinasawiri mazingira halisi ya kijamii. Mathalani, katika tamthiliya ya *Tambueni Haki Zetu* uk. 1, Mwandishi anasema:

> MIZIMU: Sekulu! Waheshimiwa wa kuzimu, mwitikieni Mundewa, mwingizeni kutoka kuzimu ajiunge na babu zake, astarehe milele.
>
> SEKULU: …Wazee wa kuzimu wamekataa damu ya Wakusi wengi inakulilia. Damu hiyo iko juu ya kichwa chako, mikono yako ina damu, miguu yako ina damu, mwili wako wote una damu. Huwezi kuingia kuzimu ...*(*uk. 1).

Hapa mwandishi ametumia mizimu na kuzimu kuonyesha kwamba Waafrika wanaamini kuhusu kuwapo kwa mizimu na kuzimu. Kwa kuzingatia Ontolojia ya Kibantu, suala la mizimu lipo hadi sasa, ambapo jamii nyingi bado zinaabudu na kutukuza mizimu, kupitia majina wanayopewa watoto na ibada (Mulokozi, 2017). Katika tamthiliya ya *Tambueni Haki Zetu,* uhalisia wa maisha katika jamii unapewa msingi mkubwa wa uandishi. Hapa Penina Muhando amechangia kuelimisha jamii kuthamini tamaduni zetu na anawataka wanajamii waandike kazi kwa kujikita katika muktadha halisi wa kijamii. Vilevile Muhando amekuwa na mchango mkubwa katika kuhamasisha masuala ya Kijinsia kupitia kazi mbalimbali alizoziandika na kupitia mashirika mbalimbali aliyowahi kufanya kazi.

**Kuhamasisha Masuala ya Usawa wa Kijinsia**

Usawa wa kijinsia ni namna ya kuonesha kuwa mwanamke na mwanamume ni sawa, na jambo lolote linalotengua usawa huo sharti lizuiliwe. Masuala ya usawa wa kijinsia yalijihusisha na harakati za ukombozi wa mwanamke, ambazo zilianza miaka ya 1975 baada ya umoja wa Mataifa kutangaza kwamba ni mwaka wa wanawake duniani (Muhando, 1982; Mahenge, 2010). Muhando (1982) aliandika tamthiliya ya *Nguzo Mama* ili kuhamasisha jamii kujihusisha katika ukombozi wa mwanamke katika mikatale ya unyonywaji, kukandamizwa, na kubaguliwa ndani ya jamii. Kadhalika, aliandika vitabu vingine vinavyohusu masuala ya usawa wa kijinsia na namna ya kumwinua mwanamke, ambavyo ni *Gender Responsive Pedagogy: a teacher's hand book* (2005), *Empowering Youth through TUSEME, Let us speak out: a teacher's handbook* (2005), *The Gender Responsive School: A handbook for education practitioners* (2005). Lengo ni kuitaka jamii ihusike katika kuleta usawa wa kijinsia. Penina Muhando kupitia tamthiliya ya *Nguzo Mama,* alionyesha changamoto na vikwazo mbalimbali vinavyokwamisha ukombozi wa mwanawake. Kama tuonavyo hapa:

BI NNE: Haya vutaaa! [*wanavuta kwa wimbo wa kazi*]
BI TATU: Jamani mie naondoka. Mnaiona Volvo hiyo imenifuata mie.
BI NANE: Wacha utani aisee tufanye kazi
BI TATU: Siyo utani ndugu yangu. Tunakwenda kwenye pati ya mume wangu leo saa moja. ...
BI NANE: Basi tuendelee kidogo bwana.
BI TATU: Unasema hivyo kwa vile wewe una kazi ya mshahara... (Uk. 41).

Kupitia mazungumzo ya Bi. Tatu katika dondoo hilo, tunabaini kwamba Bi. Tatu anaamini kuwa mwanamume ndiye kila kitu. Kwa kifupi, mwanamke wa namna hii hawezi kuwa msaada katika ushiriki wa harakati za ukombozi wa mwanamke. Hivyo, kupitia mawazo ya Bi. Tatu, mwandishi anatufahamisha kwamba ukombozi wa mwanamke lazima uanze na mwanamke mwenyewe kutambua nafasi na wajibu wake kama binadamu huru asiye tegemezi. Hali hii inatokana na uhalisia wa mazingira yaliyomlea na kumkuza, yaani mazingira ya jamii yake. Kimsingi, tamthiliya hii imebainisha vikwanza mbalimbali vinavyozuia usawa wa kijinsia ambavyo vinapaswa kuondolewa. Kupitia kwa mhusika Chizi (uk. 47-57), mwandishi anaonesha kuwa suala la ukombozi wa mwanamke linapaswa kuhusisha jamii nzima. Kadhalika, amesaidia kuelimisha jamii kupitia kazi zake na mradi wa TUSEME na FAWE kuhusiana na usawa wa kijinsia na namna ya kumwinua mtoto wa kike. Ndio maana Muhando aliandika kazi zenye kutmia mbinu za utambaji wa kingano ili kuakisi mazingira ya kijamii.

**Miongoni mwa Wanzilishi wa Tamthiliya ya Kiswahili ya Majaribio**

Watunzi wengi wa tamthiliya ya Kiswahili wanaiga mbinu na kanuni za tamthiliya ya Ulaya, hasa ya ki-Aristotele (Mulokozi 2017). Hivyo, kisanaa tamthiliya zao hazikutofautiana na tamthiliya za Kiingereza, hasa za kihalisia. Tofauti yao na watunzi wa Ulaya iko katika maudhui na lugha inayotumika. Watunzi wachache akiwemo Ebrahimu Hussein na Penina Muhando hawakuridhika na ukopaji huu; waliona kuwa palihitajika tamthiliya ya Kiafrika yenye kuchota mbinu zake kutoka katika sanaa za jadi za Kiafrika. Hivyo, watunzi hao walianzisha maigizo ya majaribio. Penina Muhando kupitia tamthiliya zake, hususani *Lina Ubani* na *Nguzo Mama* ametumia utambaji wa kingano na majigambo. Lengo la majaribio haya ni kuifanya tamthiliya ya Kiswahili ioane na utamaduni na mazingira ya Kiafrika. Hivyo, amechangia katika kuanzisha fasihi ya Kiswahili ya majaribio, ambayo ilihusu kuingiza fani mpya katika tamthiliya. Kuingizwa kwa fani hizi katika fasihi ya Kiswahili kulijulikana kama majaribio katika fasihi ya Kiswahili. Mara nyingi mtindo ndio unaomtofautisha mwandishi mmoja na mwingine maana ndio unaodhihirisha ufundi na upekee wa msanii (Mulokozi, 2017). Baadhi ya vipengele vya mtindo vilivyotumika katika tamthiliya za Penina Muhando ni: Mtindo wa diolojia, yaani wa majibizano (mazungumzo) ambapo ndani yake kuna mbinu mbalimbali zenye kuchota baadhi ya vipengele vya fasihi simulizi, kama vile nyimbo, ngoma, na matumizi ya hadithi ndani ya tamthiliya. Mathalani katika tamthiliya ya *Lina Ubani* mwandishi amemtumia mhusika Bibi na Mtambaji katika kutamba hadithi ndani ya kazi yake. Kwa mfano, katika (uk. 2 - 3), amemtumia Mtambaji kama mhusika akianza kusimulia hadithi kumhusu Bibi na familia yake, kama inavyojibainisha hapa chini:

MTAMBAJI: Paukwa!
HADHIRA: Pakawa!
MTAMBAJI: Paukwa!

HADHIRA: Pakawa!
MTAMBAJI: Hapo zamani za siku hizi
Palitokea huyo bibi…

Hapa tunaona mwandishi ametumia mtindo wa mianzo na miisho ya kifomula ili kuvuta usikivu wa hadhira. Mtambaji amejitokeza kila mara ama katika kila onyesho. Lengo la mtambaji ni kusisitiza maudhui yaliyomo katika tamthiliya husika. Pia, humfanya msomaji kuendelea kufuatilia mchezo ama igizo husika. Mathalani, mwishoni mwa tamthiliya ya *Lina Ubani* (uk. 59), Kwa ujumla, mbinu ya usimulizi inapotumika katika tamthiliya huambatana na nyimbo na humsaidia wasomaji ama hadhira kuwa makini katika kuifuatilia hadithi ama simulizi husika. Kutokana na majaribio kama haya tumeweza kupata aina ya tamthiliya inayosawiri mazingira ya kijamii ijlikanayo kama thieta ya umma.

**Mwanzilishi wa Thieta ya Umma**
Penina Muhando ndiye mwanzilishi wa Thieta ya Umma[6] nchini Tanzania (miaka ya 1970 na 1980) (Mulokozi 2017). Thieta ya umma ni aina ya sanaa za maonyesho iliyoigizwa moja kwa moja na wanajamii wa eneo fulani, wakishirikiana na wataalamu wa Sanaa kwa lengo la kuyaakisi matatizo ya watu wa eneo husika na kuyatolea suluhisho (Muhando, 1991). Thieta ya umma huweza kuchukuliwa kama juhudi ya kuibua aina ya thieta yenye kusadifu maisha na harakati za watu wenyewe dhidi ya thieta ya burudani inayokwepa uhalisi wa matabaka ya watawala. Muhando amechangia kwa kiasi kikubwa katika uandishi wa sanaa za ukumbini au thieta kwa maendeleo ya jamii. Thieta ya umma ilikuwa tofauti kabisa na thieta za Wazungu. Wakoloni walisema Afrika hakuna sanaa za ukumbini au thieta. Hii ni kwa kuwa thieta yao ilihusu kukaa katika ukumbi na watazamaji wamekaa kwenye viti wakitazama wasanii wakiigiza peke yao. Pia, walitoa kiingilio. Thieta ya umma ilikuwa tofauti na hiyo ya Wazungu, kwani iliendeshwa na jamii kwa kuingiza sanaa za Kiafrika kama vile ngoma, nyimbo, sarakasi na maigizo. Aidha, walizunguka maeneo mbalimbali kama Msoga, Bagamoyo mjini, Mkambalani Morogoro, na Malya huko Mwanza[7]. Thieta hii ililenga kutatua matatizo ya jamii kwa kufanya tafiti mbalimbali, kisha wananchi wanashiriki katika kufanya tafiti hizo. Wananchi walikuwa watendaji wakuu wa thieta. Jambo hili lilisisimua sana na kufanya thieta hii kuwa maarufu. Hapo aliwathibitishia Wakoloni (Wazungu) kuwa Afrika kuna thieta, ambayo ni tofauti na ya kwao. Hii inatokana na ukweli kwamba Wazungu waliwadharau Waafrika, kwani waliwaona ni nusu watu, na kwamba hawana thieta (Mulokozi, 2017). Kama wasemavyo wanauhalisia ni kuwa sanaa iwakilishe ukweli na kuwakilishwa kwa maneno halisi, iwe aminifu na ionyeshe hali halisi ya mazingira (Lukacs, 1963). Kupitia nadharia hii, Muhando amefanikiwa kuangazia mambo mbalimbali kwa kuakisi hali halisi ya jamii yake. Pia thieta ya Kiswahili na Kiafrika kama somo lilianzishwa na Muhando na ndiye alikuwa mwalimu wa kwanza wa somo hilo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Katika mahojiano yaliyofanywa na mtafiti na mtafitiwa mwaka 2020, ilibainika kuwa hadi mwaka huo, somo hilo linasomwa katika chuo hicho na ni sehemu ya fasihi ya Kiswahili. Aidha, wataalamu wengi wa thieta wameongezeka na kufanya sanaa hii kukua na kupendwa zaidi. Sanaa ambayo imesaidia wanafunzi wengi kuwa wabunifu wa kazi mbalimbali za fasihi. Mathalani Elizabeth Mahenge ni mwaafunzi Mhando ameandika tamthiliya za Kiswahili takribani kumi. Tamthiliya zinazotungwa na waandishi hawa zinaakisi tamaduni za Kiafrika kutokana na kutokana na kuchota mbinu zake kutokana na sanaa za jadi za Kiafrika. Aidha kutokana na ubunifu wa Penina Muhando ameweza kaanzisha nadharia zinazotumika khahiki kazi za fasihi hususani tamthiliya ya Kiswahili.

[6]Thieta ya Umma ni aina ya sanaa za maonyesho ambayo haifungwi na muundo wa Kiaristotle.
[7]Mahojiano yaliyofanywa baina ya mtafiti na mtafitiwa nyumbani kwake Kunduchi mwaka 2020.

### Mwanzilishi wa Nadharia za Kifasihi

Penina Muhando amesaidia katika kutunga na kuanzisha nadharia za kitaaluma katika fasihi. Kwa mfano, Nadharia za Drama, Nadharia ya Sanaa za Maonyesho, na Nadharia za Thieta ya Umma. Kwa kutoa nadharia hizi, Penina amesaidia kuendeleza taaluma ya fasihi. Kwa mfano, Nadharia za Drama wakati wa ukoloni waliiga mbinu na kanuni za tamthiliya za Ulaya, hasa ya ki-Aristotele. Miaka ya 1970 watunzi wachache hawakuridhika na ukopaji huo. Miongoni mwao ni Ibrahimu Hussein na Penina Muhando. Hivyo, watunzi hao walianzisha maigizo ya majaribio. Penina Muhando alifanya majaribio ya kuifanya tamthiliya ioane na utamaduni pamoja na mazingira ya Kiafrika. Pia, alitumia mbinu za utambaji wa ngano katika maigizo, ambazo ziliifanya Nadharia ya Drama kusadifu mazingira halisi ya jamii husika. Kuhusiana na Nadharia ya Sanaa za Maonyesho, Muhando na Balisidya (1976) walieleza kuhusu chimbuko la sanaa za maonyesho na kuelezea mambo yanayotakiwa katika Sanaa za maonyeho, ambayo ni dhana inayotendeka, mtendaji, uwanja wa kutendea, na watazamaji. Pia, walibainisha nadharia tatu za chimbuko la sanaa za maonyesho, ambazo ni miviga, umithilishaji, na kuwepo kwa sanaa za maonyesho za kijadi. Kadhalika, Muhando (1991) alianzisha thieta ya umma, ambayo ilifahamika kama sanaa kwa maendeleo ya jamii. Thieta ya umma ni Sanaa ya watu kwa ajili ya watu na inaiondoa tamthiliya ya Kiswahili katika mkondo wa tamthiliya za Ulaya na kuiweka katika utamaduni na mfumo wa Sanaa za Maonyesho za Kiafrika, hususani zile za tabaka la wanyonge (Mulokozi, 2017). Nadharia ya Thieta ya Umma ilizingatia vipengele vifuatavyo: nyimbo na ngoma, lugha sadifu kulingana na mazingira, maudhui yanayoakisi maisha na matatizo ya watu wenyewe, ushirikishwaji wa mtu yeyote katika sanaa na matumizi ya ishara, maigizo-bubu na mbinu nyingine za kijadi. Kwa kutoa nadharia hizi, Penina amesaidia kukuza na kuendeleza taaluma ya fasihi ya Kiswahili. Kama asemavyo Leo (2016) kuwa tamthiliya imeendelea kukua na kwa sasa kuna mchepuo wa tamthiliya ujulikanao kama filamu ambao umechukua nafasi ya tamthiliya na kuwa ndiyo sanaa ya umma ya maigizo kwa Kiswahili. Kupitia kazi zake Muhando nadharia hizo zimesawiriwa vyema.

### Hitimisho

Mchango wa Penina Muhando katika fasihi ya Kiswahili unapatikana katika vipengele vya fani na maudhui, hasa kwa kujikita katika matumizi ya lugha, kuchochea ubunifu kwa waandishi chipukizi, kuingiza maudhui ya dini za Kiafrika katika fasihi na kuhamasisha masuala ya usawa wa kijinsia. Pia kuanzisha Thieta ya Umma, Fasihi ya Majaribio ya Kiafrika, somo la Thieta ya Kiswahili na Kiafrika pamoja na nadharia za fasihi ya Kiswahili. Vipengele hivyo vyote vina mchango mkubwa katika maendeleo ya fasihi ya Kiswahili. Kimsingi, Muhando alipenda mabadiliko katika sanaa ya tamthiliya, hivyo alijaribu kuibua mbinu mpya za utunzi wa tamthiliya ili kuakisi mazingira halisi ya Kitanzania. Kwa ujumla, mwandishi huyu amefanikiwa kutoa mchango mkubwa katika fasihi ya Kiswahili na jamii kwa ujumla. Aidha, vitabu vyake vyote alivyotunga vinaenda sambamba na uhalisia wa jamii. Kadhalika, amesaidia kuelimisha jamii kupitia kazi zake na mradi wa TUSEME na FAWE kuhusiana na umuhimu wa elimu kwa watoto wa kike.

### Marejeleo

Caleb, C. W. (2013). *Taswira ya Mwanamke katika Tamthiliya ya Nguzo Mama na Mama Ee* (Tasinifu ya Shahada ya Umahiri). Chuo Kikuu cha Nairobi.

George, G. (2014). *Usawiri wa Mwanamke katika Tamthiliya Teule za Penina Muhando* Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Dodoma, Dodoma.

Hegel, G. W. F. (1979). *Hegel's System of Ethical Life and First Philosoph of Sprit*. State University of New York Press.

Mapunjo, G. C. (2014). *Usawiri wa Mwanamke kama Kiongozi katika Tamthiliya: Uchunguzi wa Kivuli Kinaishi na Nguzo Mama*. Tasinifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, Dar es Salaam.

Mbiti, J. S. (2011). *African Religions and Philosophy*. Third Edition. East African Educational Publishers Ltd.

Mlama, P. (1983). "Utunzi wa Tamthiliya katika Mazingira ya Tanzania" katika TUKI. *Makala za Semina III*.

Muhando, P. (1972). *Hatia*. East African Publishing House.

Muhando, P. (1973). *Tambueni Haki Zetu*. Tanzania Publishing House.

Muhando, P. (1982). *Nguzo Mama*. Dar es Salaam University Press.

Muhando, P. (1984). *Lina Ubani.* Dar es Salaam University Press.

Muhando, P. (1991). *Culture and Development: The Popular Theatre Approach in Africa*. Scandinavia Institute of African Studies.

Muhando, P. (2005). Empowering Youth through TUSEME, let us speak out: Teacher's handbook.

Muhando, P. (2005). Gender Responsive Pedagogy (et al) FAWE. Nairobi Publisher

Mulokozi, M. M. (2002). *The African Epic Controversy: Historic, Philosophical and Aesthetic Perspectives on Epic Poetry and Performance*. Mkuki na Nyota Publishers.

Mpalanzi, L. (2018). Mpaka kati ya Uganga na Uchawi: Uchunguzi kutoka Riwaya za Kiethnografia za Kiswahili. *Mulika Na. 17.*

Mulokozi M. M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. KAUTU.

Mutembei, A. K. (2012). *Nadharia ya Korasi*. TUKI.

Nicholaus, A. (2011). "Falsafa ya Ubuntu Ilivyosawiriwa katika Tamthiliya Teule za Penina Muhando." (Tasinifu ya Umahiri). Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Sayi J. (2023). "Matumizi ya Taswira Yanayoibua Ujumbe katika Tamthiliya ya *Nguzo Mama* (1982) (Tasnifu ya Uzamili) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Vide Muwa Press

Wamitila, K. W. (2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Focus Books.

Sayi, J. (2023). "Matumizi ya Taswira Yanayoibua Ujumbe katika Tamthiliya ya *Nguzo Mama* (1982). Tasnifu ya Uzamili: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (Haijachapishwa)